
Kuona
Kuhukumu
Kutenda

Toleo la 1. Agosti 2016

**Kimetolewa na:** TUSHIKANE e.V.;
CAJ - Jimbo la Würzburg na
Taasisi ya Joseph Cardijn,
Würzburg, Ujerumani.

**Kinapatikana:** UVIKAMBI Center
Parokia St. Alois
P.O. Box 94 Mbinga
Ruvuma Region
Tanzania

**Mwandishi:** Stephen Makinya, Mag. Theol. Kwa miaka mingi alikuwa mlezi wa kiroho wa Vijana Wakristo Wafanyakazi (CAJ) ngazi ya Taifa, Ujerumani. Anaishi na kufanya kazi Ujerumani.

**Muasisi:** Pd. Nikolaus Hegler, Paroko wa Parokia ya Johannesberg-Glattbach, Ujerumani. Kwa miaka mingi alikuwa mlezi wa kiroho wa Vijana Wakristo Wafanyakazi (CAJ) Jimbo la Würzburg. Ni mwanzilishi wa ushirikiano wa kidugu kati ya CAJ Würzburg na UVIKAMBI.

**Chapa:** Benedict Press Vier-Türme GmbH,
D-97359 Münsterschwarzach,
www.benedictpress.de

# Kuona - Kuhukumu - Kutenda

## Njia ya kutathmini kwa kina maisha binafsi na matukio katika jamii na jinsi ya kuyabadili

TUSHIKANE e.V.

CAJ

Taasisi ya Joseph Cardijn

***„Maisha yasiyotafakariwa hayafai kuyaishi“***

*Socrates, Mwanafalsafa wa Kiyunani, 469-399 KK*

# Utangulizi

Kijitabu hiki kidogo hakikusudii kutoa nadharia ya njia ya KUONA-KUHUKUMU-KUTENDA, bali ni kitendea kazi kinachoweza kulinganishwa na jembe: Ukiliweka kwenye kona la nyumba tu lipumzike usiku na mchana, halitakufaa chochote.

Vivyo hivyo kijitabu hiki kitazaa matunda tu endapo kitatumika kama mwongozo katika mijadala na tathmini za mada au matukio mbali mbali katika jamii na si kuwekwa kama pambo kwenye kabati la vitabu majumbani.


Stephen Makinya

Würzburg, Ujerumani, Agosti 2016

# Yaliyomo

1. Historia fupi ya Kuona-Kuhukumu-Kutenda
2. Kuona-Kuhukumu-Kutenda
3. Mifano
4. Maswali muhimu
5. Sala ya Vijana Wafanyakazi Wakristo
6. Misemo ya Joseph Cardijn

# 1. Historia fupi ya Kuona – Kuhukumu – Kutenda




*Kardinali Joseph Cardijn, mwanzilishi wa njia ya Kuona-Kuhukumu-Kutenda*

Padre Joseph Cardijn aliyezaliwa tarehe 13.11.1882 katika kijiji kidogo cha Schaarbeek huko Ubelgiji ndiye aliyeanzisha njia hii ambayo leo inatumika katika sayansi zote za jamii.

Ni padre aliyetoka kwenye familia maskini aliyejitolea maisha yake yote kusaidia kuboresha maisha ya vijana wafanyakazi viwandani. Miaka hiyo mapinduzi ya viwanda Ulaya yalikolea moto. Viwanda vingi vilihitaji wafanyakazi wengi. Kilikuwa kipindi kigumu kwa wafanyakazi wote viwandani, hasa vijana. Mazingira ya kazi yalikuwa magumu: Kelele nyingi za mashine, kazi nzito za kutumia mikono

kama kubeba vyuma, masaa mengi ya kazi (hadi 14 kwa kutwa), kufanya kazi usiku, kutopewa likizo na malipo kidogo sana. Mazingira haya magumu ya kikazi yaliathiri afya za vijana na pia maadili yao.

Licha ya kuwa na kipato kidogo, wazazi wa Cardijn walijitolea sadaka ili mtoto wao aendelee na masomo ya sekondari na chuo kikuu badala ya kuanza kazi viwandani kama ilivyokuwa kwa rafiki zake wengi wa umri wake.

Kila aliporudi nyumbani wakati wa likizo alijionea jinsi vijana wenzake walivyokuwa wakiteseka kwa kazi nzito. Rafiki zake wa zamani walimwonea wizu, wakamcheka kama "legalega" na kumtenga wakisema si mmoja wao. „Anajifanya msomi". Hii ilimwuuma.

Kabla ya kufa baba yake Cardijn alimwahidi baba yake kuwa atatolea maisha yake yote kusaidia vijana wafanyakazi .

Baada ya kupewa daraja la upadre mwaka 1906 alianza mara kutekeza ahadi yake ya kulitumikia tabaka la wafanyakazi viwandani. Ingawa haikuwa kawaida kwa mapadre wakati huo kuwatembelea wafanyakazi viwandani kwa madai kuwa ni watu wa tabaka la chini, Cardijn "alivunja" desturi hiyo kwa ushujaa. Mara kwa mara alikwenda kwenye lango la viwanda na kuwatakia hali vijana waliotoka baada ya kumaliza kazi nzito. Pia alizitembelea familia maskini za wafanyakazi kujua hali zao na kuzifariji.

## 1.1 Aanzisha Umoja wa Vijana Wafanyakazi Wakristo (YCW)

Cardijn aliamini kwa dhati kuwa mabadilio ya kweli yataletwa tu na watu wenyewe wanaoathiriwa na hali halisi na siyo mwingine. Sharti muhimu ni kwamba waungane.

Ndiyo maana mwaka 1925 alianzisha Umoja wa Vijana Wafanyakazi Wakristo (Young Christian Workers, YCW) akiwa na vijana wachache tu waanzilishi. Hadi alipokufa mwaka 1967, YCW ilikuwa imekwisha enea nchi zaidi ya 100 duniani. Lengo kubwa la umoja huu lilikuwa ni kuwasaidia vijana, licha ya mateso makubwa viwandani au mazingira yoyote wanayoishi, watambue hadhi yao kama watoto wateule wa Mungu na kusimama kidete kubadili hali ya maisha, jamii na mfumo unaowakandamiza. Mbiu yake muhimu hadi leo ni: *"Kila kijana mfanyakazi ana thamani kubwa zaidi kuliko dhahabu yote ya dunia nzima, sababu ni mtoto wa Mungu."*

Ili kufikia lengo hilo la mabadiliko ya kweli, Cardijn alibuni njia ya **Kuona, Kuhukumu, Kutenda** na kuwapa vijana wake kama nyenzo ya kujikwamua toka maisha ya ukandamizwaji. Alia-amini kuwa hatua hizi zikifuatwa vizuri zitawasaidia vijana kutafakari na kuchambua kwa kina hali halisi



*Vijana wakiwa kwenye mjadala*

inayowakabili *(Kuona),* athari zake *(Kuhukumu*) na kubuni njia za kuibadili (*Kutenda).*

Vijana hao walikutana kwenye vikundi vidogo vidogo mara moja kwa wiki ili kutafakari maisha yao na ya jamii yao.

Kila mmoja alipata fursa ya kusimulia jambo moja lililomtokea na kumgusa katika wiki hiyo alilodhani ni vema kuwashirikisha wenzake. Tukio hilo laweza kuwa lilitokea kazini, nyumbani, shuleni, au mahali pengine popote.

## 1.2 Kwa nini aliunda Umoja wa Vijana Wafanyakazi Wakristo (YCW)

Cardijn aliamini kuwa mabadiliko ya kijamii hayawezi kutokea kwa nguvu ya mtu mmoja mmoja peke yake. Aliaamini kuwa yatatokea endapo vijana wataungana pamoja na kubuni mbinu za kuyaleta.

Kifupi: Asilia njia hii ilitumika kama chombo cha kutathmini hali halisi iliyowakumba vijana waliokuwa wanafanya kazi kwenye mazingira magumu ya viwanda huko Ubelgiji. Lengo lake likiwa ni kubadili hali hiyo ili iendane na hadhi ya wafanyakazi hao kama watoto wa Mungu. Hivyo kimsingi mada iliyotakiwa kuchambuliwa kwa njia hii ni tatizo, hali isiyoridhisha au changamoto vilivyowakabili waathiriwa. Lengo lake likiwa kupanga mkakati wa pamoja kuitatua au kuibaidili hali hiyo.

Ingawa mada inaweza kuhusu pia maisha binafsi, kwa kiasi kikubwa jamii au mfumo ndivyo vilivyokuwa walengwa wa kwanza wa uchambuzi huu hapo mwanzoni. Kama tulivyoona huko juu, mazingira ya kikazi ya viwandani ndiyo yalikuwa mada kuu kwenye mikutano ya vikundi vidogo vidogo vya waanzilishi wa Umoja wa Vijana Wafanyakazi Wakristo.

## 1.3 Matumizi ya njia hii leo

Kihistoria njia hii imeleta mapinduzi makubwa katika harakati za kupigania haki za wafanyakazi. Vyama vingi vya wafanyakazi duniani (Trade Unions) vimefanikiwa kwa kutumia njia hii kupigania haki za wafanyakazi ambazo kwa sasa zinatambuliwa rasmi na Umoja wa Mataifa kama haki za kimsingi za kila mfanyakazi popote duniani.

Leo hii karibu sayansi zote za jamii na nyanja mbali mbali kama vile siasa, dini, uchumi, n.k. huitumia njia hii baada ya kuiona kuwa ni njia mahususi ya kitaalamu kuchambua kwa kina mambo au matukio katika jamii na kubuni njia za kuyarekebisha.

Njia hii inaweza kutumiwa na *mtu binafsi* (mfano katika harakati za kujipangia malengo ya maisha), *Vikundi vya watu* (mfano umoja wa vijana, vyama vya ushirika, n.k.) *, idara na taasisi* mbali mbali, *asasi* sizizo za kiserikali, *vyama* vya kisiasa, n.k.

**Kifupi:** Hakuna jambo au tukio lisiloweza kuchambuliwa kwa kutumia njia hii.

## 1.4 Faida zake

- ✓ Ni njia rahisi isiyohitaji utaalamu wa pekee kuitumia.
- ✓ Inaweza kutumika kuchambua kila jambo au tukio.
- ✓ Inasaidia kuchambua mambo kwa kina hivyo kutuepusha kuhukumu au kutenda mambo kwa pupa.
- ✓ Ni ya vitendo: Inambana mshiriki hadi aseme nini kitafanyika kutatua tatizo. Kifupi: Kila tathmini halisi lazima mwisho wake ijibu swali: "Kitu gani kifafanywa na nani na hadi lini ili kubadili hali hiyo?"
- ✓ Inatia moyo kwa kuwa lengo lake kila mara ni kubadili hali iwe nzuri zaidi.

## 1.5 Ni hatua tatu zinazojitegemea

Kama ilivyosemwa hapo awali, lengo kubwa la njia hii ilikuwa ni kuwawezesha vijana watafakari kila jambo kwa kina na si kwa kuruka ruka tu. Ndiyo maana licha ya kuwa ni njia moja, ina hatua tatu zinazojitegemea: Kuona, Kuhukumu, Kutenda. Kimsingi hairuhusiwi kuanza hatua inayofuata kabla ya kujihakikishia kuwa hatua iliyotangulia imefanywa vizuri hadi mwisho.

Hii inatofautiana na mtindo wetu wa utendaji katika maisha ya kawaida: mara nyingi watu wengi wakisikia kitu, kabla ya kuchunguza kwa ndani kitu gani kimetokea na kwa nini (kuona), hukimbilia hatua ya tatu „tufanye nini?" (kutenda). Matokeo yake mara nyingi ni kutoa suluhisho la haraka ambalo baadaye linaweza kuonekana kuwa linasababisha hasara ambazo mtu wakati wa uamuzi wa haraka hakuziona.

**Mfano:** Inahisiwa kuwa uchafu toka kiwandani unasababisha vifo vya samaki kwenye mto ulio karibu. Bila kufanya uchunguzi wa kina serikali kwa kushinikizwa na wakazi wa eneo unakopita mto huo iliamuru kiwanda hicho kifungwe mara moja. Kiwanda kilipofungwa, waajiriwa 600 walipoteza mara ajira zao.

Uchunguzi wa kina ulipofanywa baadaye ulibaini kuwa uchafu unaoingia mtoni hautoki kwenye kiwanda jirani na mto kilichofungwa bali toka kiwanda kingine kikubwa zaidi kilicho mbali zaidi.

Mfano huu unaonyesha kuwa kama uchunguzi wa kina ungefanywa kabla ya kuchukua hatua za haraka haraka, wafanyakazi 600 wasingepoteza ajira zao.

**Mfano wa pili:** Dereva wa basi kaacha ghafla barabara na kugonga nyumba iliyo pembeni mwa barabara. Walioona tukio hilo kwa mbali walikimbilia kusema: „Aisee, dereva huyo hafai kabisa!“ (kuhukumu); “ni lazima aadhibiwe kwa kuharibu nyumba“ (Kutenda).

Uchunguzi wa kina kwa njia ya Kuona-Kuhukumu-Kutenda utataka kwanza kujua kwa nini dereva aliacha barabara. Uchunguzi huo unaweza, kwa mfano, kubaini kuwa dereva aliacha barabara ghafla ili kumkwepa mtoto aliyekuwa akivuka barabara.

Mfano huu unaonyesha kuwa kama anayetoa hukumu angejitahidi kuuliza kwanza “kwa nini” dereva aliacha njia, asingekimbilia kumlaani kama mtu mbaya maana katika tukio hilo kuokoa maisha ya mtoto kulikuwa muhimu zaidi kuliko kutogonga nyumba.

# 2. KUONA-KUHUKUMU-KUTENDA

Hebu tuziangalie hatua hizi kila moja peke yake:

## 2.1 KUONA

Hatua hii tunaweza kuiita ni hatua ya “Utafiti” au “Upelelezi” na ina vipengele vinne:

Kipengele cha kwanza ni cha **“MAELEZO”** ya tukio au hali halisi, yaani kueleza kirefu iwezekanavyo na kwa ufanisi tukio **BILA KUSEMA KAMA BAYA AU ZURI!** Kama ni mada inayozungumziwa basi ni kufafanua maana ya mada.

Kipengele hiki kinajibu swali **“NINI KIMETOKEA?** Katika hatua hii washiriki wanatakiwa kumwuuliza msimliaji maswali mengi iwezekanavyo hadi wawe na uhakika kuwa wameelewa kila kitu.

Kipengele hiki ni muhimu ili kuwa na uhakika kuwa washiriki wote wameelewa fika ni jambo gani linalozungumziwa. Uelewa huo ndiyo msingi muhimu wa kuendelea na hatua nyingine.

Kipengele cha pili kinachofuata baada ya "Maelezo" tunaweza kukiita kipengele cha **"SABABU"**. Hii ni nafasi ya kutafuta sababu zinazolifanya jambo au tukio hilo liwe hivyo lilivyo kama ilivyotolewa kwenye maelezo. Kinajibu swali **"KWA NINI?"**. Jambo linaweza kusababishwa na watu, itikadi, mfumo, mazoea, n.k. Washiriki wa tathmini wajitahidi kutaja sababu zote wanazodhani zinachangia kutokea kwa tukio hilo bila kuficha. Ni muhimu sana kuweka sababu zote wazi, ili kuhakikisha kuwa wakati wa "Kutenda" suluhisho zinazopendekezwa zinawiana na sababu.

Kipengele cha tatu ni "WAHUSIKA". Katika kipengele hiki washiriki wa mjadala hujitahidi kuwataja wahusika wote katika tukio hilo na kwa jinsi gani wanahusika katika tukio hilo. Wahusika hao wanaweza kuwa watu, idara, mfumo, n.k. Mfano, kama tukio ni mazingira mabaya kikazi, wahusika ni uongozi wa kiwanda, labda sheria za haki za wafanyakazi kwenye nchi kilipo kiwanda hicho; wafanyakazi wenyewe, n.k.

Kipengele cha mwisho tunachoweza kukiita **"MATOKEO"** kinajikita kuchunguza faida au madhara yanayoweza kutokea kutokana na tukio hilo (mabaya na mazuri) na kubaini wanufaika au waathirika wake (watu, jamii, mfumo, nchi, n.k.). Kipengele hiki hujibu swali: **"MATOKEO YAKE NI NINI?"**

## Maswali muhimu katika hatua ya “Kuona“

1. Nini kimetokea, lini, na wapi?
2. Kwa nini?: Sababu mbali mbali unazodhani zimesababisha hilo.
3. Nani ni wahusika?: Watu binafsi, mfumo, idara, n.k.
4. Matokeo yake ni nini?: Nani wananufaika na hali hiyo? Jinsi gani? Nani wanaathirika na hali hiyo? Jinsi gani?

## 2.2 KUHUKUMU

Hatua hii ya pili inafuata baada ya kuhakikisha kuwa vingele vyote vya "Kuona" vimejibiwa vizuri. Kuhukumu hapa haina maana ya tamko la mwisho la hakimu mahakamani, bali **KUPIMA** jambo au tukio kwa kutumia vigezo mbali mbali ili hatimaye kutoa maoni yako kama jambo hilo ni baya au zuri.

Hatua hii ina vipengele vikuu viwili:

Kipengele cha kwanza tunaweza kukiita **„VIGEZO"**. Hiki kinawaalika washiriki wa njia hii kutathmini kwanza vigezo gani wanavitumia kupima tukio, mada au jambo husika kama zuri au baya. Vigezo hivyo vinaweza kutokana na misingi mbali mbali kama vile: Biblia au vitabu vingine vya dini, mila na desturi za mahali, maadili ya jamii husika, sheria za nchi, itikadi/imani za washiriki, katiba ya nchi, Makubaliano/Mikataba, Tangazo la Umoja wa Mataifa juu ya Haki za Binadamu, Tangazo la Umoja wa Mataifa juu ya Haki za Wafanyakazi, mafundisho ya Kanisa, dhamira binafsi za washiriki, n.k.

Vigezo hivi vitasaidia kutoa sababu kwa nini mshiriki anaona jambo hilo ni zuri au baya.

**Mfano 1: Biashara ya utumwa**

Mshiriki anaweza kusema jambo hilo ni baya na ni lazima likomeshwe kwa kigezo cha usawa wa kila binadamu kilichoko kwenye Tangazo la Umoja wa Mataifa juu ya Haki za Binanadamu; au kwa kigezo cha Usawa wa kila Binadamu mbele ya Mungu kama inavyofundisha Biblia.

**Mfano 2: Nchi kutawaliwa na nchi nyingine**
Mshiriki wa tathmini anaweza kusema jambo hilo ni baya kwa msingi wa haki za binadamu inayoipa kila nchi haki ya kujitawala yenyewe.

**Mfano 3: Amri ya kiwanda**

Kiwanda kinawalazimisha wafanyakazi kufanya kazi masaa 14 kwa siku. Mshiriki wa tathmini anaweza kusema amri hiyo ya kiwanda haikubaliki sababu inapingana na Haki za Kimataifa za Wafanyakazi au na sheria za nchi.

Ingawa katika maisha ya kawaida tunahukumu kila mara kama kitu ni kizuri au kibaya, ni mara chache huwa tunajiuliza ni vigezo gani tunavitumia kutoa hukumu hiyo. Mambo mengi huonekana kuwa wazi kama ni mazuri au mabaya. Licha ya hiyo, ni vema, hasa tunapokuwa wengi, kuafikiana kwa pamoja juu ya vigezo tutakavyotumia kutoa hukumu ya pamoja. Hii itamsadia pia kila mshiriki wa tathmini hiyo, inapobidi, kusema bayana na kwa mtu yeyote anayeuliza, ni kwa msingi gani tunadhani jambo hilo ni baya au halikubaliki.

Kipengele cha pili cha hatua ya Kuhukumu tunaweza kukiita **„LENGO AU NDOTO“**.

Ni kipengele ambacho si rahisi sana lakini cha muhimu kabisa. Baada ya kutambua kama tukio au hali halisi haikubaliwi, watathmini wanaalikwa kusema ni hali gani wanatamani waifikie wanayoweza kudhani ndiyo hali nzuri na inayokubaliwa kwao. Kinajibu swali: **“HALI GANI TUNATAKA TUIFIKIE?”**

Mfano wa hali hiyo inayotamaniwa inaweza kuwa: „Tunataka jamii ambamo kila mtu, bila kujali rangi, kabila, umri au jinsia anapata mahitaji yote muhimu ya binadamu kama chakula, mavazi, malazi, tiba, na uhuru wa mawazo.“

Hatua hii ni muhimu maana inatoa dira ya wapi jitihada za kubadili hali halisi zielekee. Bila kutamka pamoja **„LENGO“** gani tunataka tulifikie, ni ngumu kujua baadaye wakati wa „Kutenda“ ni kwa kiasi gani tumefanikiwa kufikia lengo hilo.

## Maswali muhimu katika kipengele hiki ni:

- Kitu gani ni kizuri katika hilo? Kwa nini?
- Kitu gani ni kibaya katika hilo? Kwa nini?
- Hisia zangu ni zipi katika hili? Kwa nini?
- Hali gani tungetamani tuifikie?

## 2.3 KUTENDA

Hatua hii ya mwisho na inayohitimisha tathmini yoyote halisi tunaweza kuiita hatua ya kuweka „**MIKAKATI**".

Hatua hii ndiyo inayotofautisha tathmini makini na aina nyingine za mazungumzo kama vile mijadala au „kupiga michapo/porojo". Mijadala iliyo mingi haina hatua ya „Kutenda" na lengo la michapo au porojo ni kuwafurahisha washiriki na siyo kufikia hatma ya kutaka kubadili hali.

Hatua ya kutenda ina vipengele viwili:

Kipengele cha kwanza tunaweza kukiita **„NINI KIFANYIKE"**. Lengo lake ni kuwaalika watathmini kubuni juu ya nini kifanyike ili kufikia lengo ambalo washiriki wanataka kulifikia kama walivyolibainisha kwenye hatua iliyotangulia ya kuhukumu. Kinajibu swali: **„TUFANYE NINI KUBADILI HALI HIYO?"**

**Mfano: Kiwanda kinawalazimisha wafanyakazi kufanya kazi masaa 14 kwa siku**

**Mkatakati:** Kupepeleza sheria za nchi zinasema nini juu ya masaa ya kufanya kazi viwandani. Ikibainika kuwa amri ya kiwanda ni kinyume na sheria ya nchi, kuvitaarifu vyombo vya serikali

vinavyohusika juu ya ukiukwaji wa sheria katika kiwanda husika na kudai hatua za haraka zichukuliwe.

Kipengele cha pili tunaweza kukiita „**MBINU AU JINSI**“. Kinawaalika watathmini kubuni mbinu za kutekeleza mikakati ya kubadili hali hiyo. Katika kipengele hiki washiriki wa tathmni lazima wajibu maswali yafuatayo:

- ✓ **NJIA AU MBINU GANI ZITUMIKE?**
- ✓ **VITU/RASLIMALI GANI TUNAHITAJI KUWA NAVYO KUFANYA HIVYO?**
- ✓ **NANI ATAFANYA NINI?**
- ✓ **HADI LINI?**

**Mfano: Kiwanda kinawaamuru wafanyakazi kufanya kazi masaa 14 kwa siku.**

*Mbinu:*

i) Kupiga simu wizara ya kazi na ajira kuulizia juu ya sheria za nchi katika suala hilo.

ii) Kuandika barua ya wazi gazetini kulaani kitendo hicho.


*Nani?* Juma na Hadija.

*Hadi Lini?* Tarehe 25.11.2016.

**<u>Maswali Muhimu katika hatua ya „Kutenda“</u>**

- Nini kifanyike ili kuibadili hali tuliyoiona na kufikika hali tunayuitaka?
- Jinsi gani?
- Nani atawajibika kufanya nini? – binafsi, kikundi, jamii, serikali, n.k.
- Zana zipi zinahitajika?
- Hadi lini tutekeleze hili?
- Vigezo vipi tutatumia kupima kama tumetekeleza vizuri jambo hilo?

# 3. MIFANO INAYOONYESHA JINSI NJIA HII INAVYOTUMIKA



*Mahakamani*

## 3.1 Kuhukumu Kesi

Ingawa hakuna anayesema wazi, hakimu ye yote hutoa hukumu ya kesi kwa kutumia njia ya Kuona-Kuhukumu-Kutenda.

Kwanza lazima hakimu ajue kwa undani kitu gani kimetokea (**KUONA**). Hii ndiyo kazi ya mawakili wa sheria toka upande wa mashataka na wa mshitakiwa. Hulazimika kufanya upelelezi wa kina na mara nyingine hata kutafuta mashahidi ili

kuisadikisha mahakama kuwa kosa limetendeka au hapana. Akisha sikia maelezo toka pande zote mbili, hakimu ataangalia sheria ipi itamsaidia kuhukumu aliyoyasikia (**KUHUKUMU**). Kisha atatoa tamko la kumwadhibu au kumwachia huru mshitakiwa (**KUTENDA**).

Hakimu asiyezingatia hatua hizi hawezi kutoa hukumu nzuri.


Mfano huu wa mahakama unatuonyesha umuhimu wa hatua ya "**KUONA**". Kesi nyingi zinachukua muda mrefu sababu lazima upelelezi wa kina ufanywe kwanza. Hatua hii isipofanywa vizuri inaweza kuhatarisha watu kuhukumiwa adhabu ingawa labda hawana kosa.

Pili  mfano wa mahakama unatuonyesha umuhimu wa kuwa na vigezo wazi vya kutumia wakati wa "Kuhukumu". Hakimu haruhusiwi kutoa hukumu kwa kutumia hisia zake, bali kwa misingi ya sheria za nchi. Ili awe hakimu mzuri, ni lazima azijue sheria hizo vizuri na ajue sheria ipi inatumika kuhukumu jambo lipi.

Kama vile hakimu anavyopaswa kujua sheria kama msingi wa kutoa hukumu yake, ndivyo washiriki wa njia ya **KUONA-KUHUKUMU-KUTENDA** wanavyowajibika pia kujua misingi itakayowapa vigezo vya kuhukumu vizuri tukio au mada. Misingi hiyo yaweza kuwa biblia, maadili ya jamii, mapokeo, itikadi, haki za binadamu, mafundisho ya kanisa kuhusu maisha ya jamii, n.k.

Mwisho mfano wa mahakama unatuonyesha kuwa kilele cha njia hii ni KUTENDA. Tamko la mwisho la hakimu juu ya hatma ya kesi ndilo linalofunga kesi. Tamko hilo linaweza kuwa ni kutoa adhabu kwa mshakitwa au kumwachia huru au kuistisha kesi.

## 3.2 Kutibiwa hospitalini



*Hospitalini*

Ukichambua vizuri utabaini kuwa daktari yeyote anapomtibu mgonjwa hufuata hatua hizi tatu:

**KUONA:** Kwanza daktari huuliza mgonjwa anaumwa nini, toka lini, n.k. Kisha daktari hujitahidi kutafuta sababu za ugonjwa (Kuona: Kipengele: Sababu). Hapa anaweza kutumia njia nyingi kama vile kuchunguza dalili za ugonjwa, maelezo ya mgonjwa mweyewe; kumpima, n.k. Njia hizi zinaweza kumsaidia mganga kujua chanzo cha ugonjwa. Lakini pia kuna magonjwa mengine ambayo daktari hushindwa kujua sababu zake licha ya vipimo mbali mbali – haya humpa changamoto ya kushindwa kumwandikia mgonjwa tiba inayofaa.

**KUHUKUMU:** Kwa kuzingatia matokeo ya "Kuona" hapo juu daktari anaweza kusema chochote juu ya hali ya mgonjwa, kwa mfano kama ugonjwa ni wa hatari au hapana.

Kutegemeana na hali halisi ya mgonjwa daktari anaweza pia kusema lengo la tiba kwa mgnjwa ni nini (hali gani tunataka tuifikie): Kama ugonjwa si wa kupona, basi daktari atasema lengo ni kumpunguzia makali ya maumuvi mgonjwa au kumsaidia aishi walau siku chache (kurefusha muda wa maisha yake). Kama ugonjwa unaponyeka basi hali ambayo daktari anapenda ifikiwe ni kupona kabisa kwa mgonjwa.

**KUTENDA:** Hatua ya mwisho anayofanya daktari ni kumwandikia mgonjwa aina ya tiba inayomfaa, mfano kulazwa au aina na idadi ya vidonge anavyotakiwa kumeza kwa kutwa, n.k.

## 3.3. Mada: Kipindupindu kimekikumba kijiji chetu

**Kuona**

*Nini:* Toka juzi watu sita wamekufa kwa kipindupindu na dispensari yetu iliripoti kupokea wagonjwa wawili waliohisiwa kuwa na kipindupindu. Uchunguzi wa maabara umebaini kuwa watu hao waliathiriwa na viini vinanvyosababisha kipindupindu.

*Sababu:* Ukosefu wa maji safi; uchafu wa mazingira; mvua kubwa zilizonyesha; ukosefu wa vyoo safi na salama, n.k.

*Matokeo yake:* Watu kuugua na wengine kupoteza maisha yao. Ndugu kuwajibika kuwatunza wagonjwa na hivyo kushindwa kwenda kazini; kugharimia matibabu; kuishi kwa hofu kuwa wakati wowote kinaweza kunikumba mimi au familia yangu; uchungu wa kufiwa ndugu.

**Kuhukumu**

*Kigezo kikuu:* Haki ya binadamu ya kuishi kwenye mazingira yasiyo na magonjwa.

*Kibaya katika hilo*: Kuugua au kufa.

*Hali tunayoitamani kuifikia*: Kuishi katika mazingira yasiyokuwa na kipindupindu.

**Kutenda:**

*Nini kifanyike?* Kampeni ya kusafisha mazingira.

*Nani?* Wanakijiji wote.

*Lini?* Jumamosi hii toka saa mbili asubuhi hadi saa kumi na moja jioni.

## 3.4. Mada: Mitara imekithiri kijijini kwetu

**Kuona:**

*Nini?* Vijana wengi wanaoa zaidi ya mke mmoja.

*Sababu:* Mila na desturi (mfano: kuoa wake wengi kama alama ya utajiri au „ufalme" kwa wanaume?; watoto wengi kama raslimali ya kuzalishia mali shambani, kupanua ukoo, n.k.; wanawake kuwategemea wanaume kiuchumi, n.k.).

*Matokeo yake:* Watoto wengi wa mitara kutotunzwa na baba zao kikamilifu; baadhi ya wanawake kutelekezwa na waume zao; kukosekana upendo katika ndoa; wivu na magomvi kati ya wanawake; shikikizo kwa mwanaume kwa kuwa hawezi kuwatendea haki sawa wake zake wote na kulazimika kufanya kazi zaidi kukidhi mahitaji ya kiuchumi ya kaya zote; ugomvi wakati wa urithi wa mali ya mume; hatari ya kuenezwa magonjwa ya jinsia, n.k.

**Kuhukumu**

*Kigezo:* Upendo kati ya mume mmoja na mke mmoja kama msingi wa ndoa.

*Kitu gani kibaya katika hilo:* Kukosekana kwa upendo halisi kati ya mume na mke; hakuna usawa kati ya mume na mke.

*Hali tunayoitaka kuifikia*: Ndoa ya mume mmoja na mke mmjoa iliyojengwa kwenye misingi ya upendo na usawa kati ya mume na mke.

*Kwa nini?* Ni njia pekee inayoonyesha usawa kati ya mume na mke na itakayohakikisha uwajibikaji mzuri na usio na ubaguzi kwa mke na watoto.

**Kutenda:**

*Nini?:* Kuwaelimisha vijana juu ya umuhimu wa ndoa ya mke mmoja na mume mmoja na madhara ya mitara.

*Namna gani?:* Semina.

*Nani?:* Wenye ndoa nzuri zinazopaswa kuigwa.

*Lini?:* Kila Jumapili baada ya Ibada.

# 4. MASWALI KWA KILA HATUA

## KUONA

- Nini kimetokea, lini, wapi?
- Kwa nini?: Sababu mbali mbali unazodhani zimesababisha hilo.
- Nani ni wahusika?: Watu binafsi, mfumo, idara, n.k.
- Matokeo yake ni nini?: Nani wananufaika na hali hiyo, Jinsi gani? Nani wanaathirika na hali hiyo? Jinsi gani?

## KUHUKUMU

- Kitu gani ni kizuri katika hilo? Kwa nini?
- Kitu gani ni kibaya katika hilo? Kwa nini?
- Hisia zangu ni zipi katika hili? Kwa nini?
- Hali gani tungetamani tuifikie?

## KUTENDA

- Nini kifanyike ili kuibadili hali tuliyoona na kufikika tunachotaka?
- Jinsi gani?
- Nani atawajibika kufanya nini?
- Hadi lini?
- Vigezo vipi tutatumia kupima kama tumetekeleza vizuri jambo hilo?

## 4.1. Hatua za kufuata wakati wa mjadala wa kikundi:

- Ripoti ya utekelezaji wa makubaliano ya mkutano uliopita
- Kujadili mada kwa kutumia njia ya Kuona-Kuhukumu-Kutenda
- Nini kitafanyika?
- Nani atafanya nini?
- Hadi lini?


# 5. Sala ya Vijana Wafanyakazi Wakristu

Bwana wetu Yesu Kristu, tunakutolea siku hii ya leo, pamoja na kazi zetu, mapambano yetu, furaha na mateso yetu.
Utujalie sisi pamoja na ndugu zetu katika ulimwengu wa kazi, tufikirie kama wewe, tufanye kazi pamoja nawe na tuishi ndani yako.
Utujalie Neema ya kukupenda kwa moyo wetu wote na kukutumikia kwa nguvu zetu zote.
Ufalme wako ufike viwandani, kwenye karakana, maofisini na nyumbani kwetu.
Uwajalie wote walio hatarini leo wadumu katika Neema yako, na uwajalie marehemu wote amani yako.
Tunakuomba hasa kwa ajili ya . . . (*maombi binafsi*).

Bwana wetu Yesu Kristu, kwa upendo wako uwabariki vijana wafanyakazi.
Bwana Yesu Kristu, utukatifuze sisi pamoja na familia zetu.
Bwana Yesu Kristu, Ufalme wako ufike kwa njia yetu na kazi zetu.
Mwenye Heri Marcel Callo, shahidi wa vijana wafanyakazi wakristu, Utuombee.
Maria, Malkia wa Mitume, utuombee. Amina.
*(Sala hii ilitungwa na Kardinali Joseph Cardijn mwenyewe na inasaliwa leo kila siku na mamilioni ya Vijana wafanyakazi Wakristo duniani kote).*

# 6. Baadhi ya Misemo ya Joseph Cardijn

„Kila kijana mfanyakazi ana thamani kubwa zaidi kuliko dhahabu yote ya dunia nzima, sababu ni mtoto wa Mungu."



„Nilianza na mmoja, wawili, watatu. Nimekuwa nikianza mara nyingi sana na kila siku naanza upya. Ni lazima kuanza upya kila siku: mara 10, mara 100, mara 1000!."

„Mitume wa kwanza na wa karibu kabisa wa vijana wanyakazi lazima wawe vijana wafanyakazi wenyewe."

„Vijana wafanyakazi si watumwa, si mashine, si wanyama bali watoto wa Mungu.".

„Kanisa bila tabaka la wafanyakazi ndani yake si Kanisa la Yesu Kristu aliyesema: Nimetumwa kuwahubiria maskini Habari Njema"

„Maisha yenu ni Injili ya Tano."

„Tupo mwanzoni kabisa. Ni lazima tuanze upya. Kila siku!"

# Juu ya watoaji wa kitabu hiki

TUSHIKANE e.V. ni Taasisi isiyo ya Kiserikali iliyoanzishwa mwaka 2009 huko Würzburg, Ujerumani. Lengo lake kuu ni kusaidia miradi ya maendeleo ya jamii nchini Tanzania na hasa katika uwanja wa elimu.

Umoja wa Vijana Wafanyakazi Wakristu (CAJ) ni chama kilichoenea dunia nzima. Lengo lake kuu ni kuwaunganisha vijana katika jitihada zao za kupigania maisha bora na mazingira mazuri kazini.

Uhusiano kati ya Umoja wa Vijana Wafanyakazi Wakristu Jimbo la Würzburg (CAJ) na UVIKAMBI ulianza tangu mwanzoni mwa miaka ya 1990 na mbiu yake ni „CAJ na UVIKAMBI Kitu Kimoja". Tangu kuanzishwa ushirikiano huo hadi leo wanachama wa CAJ na UVIKAMBI wamekuwa na fursa mbali mbali za kutembeleana, kubadilishana mawazo na kuendesha miradi ya pamoja kuinua maisha yao.

Taasisi ya Joseph Cardijn ilianzishwa mwaka 2002 ili kusaidia uendeshaji wa kazi na miradi ya  shughuli za CAJ kiuchumi. Taasisi hii inasaidia miradi ya wana CAJ Ujerumani na wana UVIKAMBI Tanzania yenye lengo ya kuboresha maisha yao.